**Title: Under the Mango Trees**

**EPISODE 8**

**Author: Romie Singh**

**Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun**

**List of characters for episode 8:**

- Narrator
- Desirée
- Bella
- Eric
- Woman (in her early twenties)
- Lorraine
- Sazi
- Grandma
- Children in background
- People in background (lining up at clinic)

Hujambo na karibu kwenye sehemu ya nane katika mfululizo wa sehemu kumi za mchezo wa kuigiza katika Noa Bongo Jenga Maisha Yako kwa jina Chini Ya Miembe. Mchezo huu unahusu mpango wa uzazi.
Leo hii Eric anaendelea na wazo lake la utafiti kuhusu njia mbalimbali za kupanga uzazi kwa usaidizi mkubwa wa Desirée na dada yake, Bella. Je nyanya Linda atakubali mazungumzo ya aina hiyo yafanyike nyumbani kwake?

SIG.TUNE UP HOLD UNDER AND FADE

**NARRATOR:** April, mama yake Desirée, aliwasisitizia wakati wote watoto wake wa kike kwamba, kuwa mwanamke sio jambo rahisi. Desirée na Bella watalazimika kujitahidi sana iwapo hatataka kuwa kina mama wa nyumbani na kazi yao iwe kuzaa mtoto mmoja baada ya mwingine kama alivyokuwa yeye. Bella alishachukua hatua ya kwanza amehama nyumbani na anaishi na mpenzi wake Robert. Kinyume na nyanya Linda alivyotaka, Bella hakutaka kuanza kupata mtoto mara tu alipoanza kuishi na mpenzi wake, analizungumzia wazo lake hilo wazi pamoja na Eric na Desirée , huku Eric akiandika maelezo hayo kwa ajili ya utafiti wake.

**<u>Sc.1 Interior. Afternoon ambience.</u>**
**SFX: Background birds/children**
**FADE IN DIALOGUE**

1. BELLA: Kliniki iliyo karibu na hapa iko katika mji wa Kentown. Iko kilomita 20. Kutoka hapa. Hiyo inamanisha ni safari ya saa nzima kwa basi. Kwa hivyo mimi nilitafuta njia ya uzazi ambayo haingenihitaji kwenda Kentown mara kwa mara. Nilitafuta njia ambayo baadae ningeweza kupata mtoto iwapo nataka.

2. DESIRÉE : Je hukutaka kutumia njia za kienyeji kama nyanya Granma Linda anavyopendekeza?

| | |
|---|---|
| 3. BELLA: | Sikutaka, Kwa sababu hazina uhakika, Well. Utafahamu baadae, Des, kuwa njia hiyo inahitaji kuacha kufanya mapenzi kabisa wakati Fulani, unaona hiyo inaweza kuleta shida. Siju ni wakati gani niko salama au wakati gani siko salama kufanya mapenzi. |
| 4. DESIRÉE: | Mimi pia. Siku zangu za mwezi zinabadilika badilika. |
| 5. BELLA: | Haswa! Mara nyingine mimi nina mzunguko wa siku 28; na mara nyingine siku 32; kwa hivyo nashindwa nitahesabu vipi kujua siku hizo mbili wakati ambapo mayai yanajenga rutuba? |
| 6. DESIRÉE : | Mwalimu wetu alituambia kwamba, huwa mtu anasikia kama anatekenywa upande mmoja wakati huo wa mayai yanapojenga rutuba. Umeshawahi kuhisi namna hiyo? |
| 7. BELLA: (laughing) | Hata! Mimi nisingetaka kubahatisha. Sitaki kupata mimba kwa sasa. Niliondoka nyumbani kwa sababu nilitaka kuwa na utulivu, ili nipate kusoma. Kwa hivyo nilihitaji kinga ya uzazi. Ndio maana mama yako Eric, daktari Alice, alipokuwa na msaada mkubwa kwangu. |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | ERIC: | Na yeye? A;ipendekeza nini? |
| 9. | BELLA: | Ndipo aliponieleza kuhusu Koili, Sindano. Na “ Diaphragm” aina nyingine ya Koili yenye umbo kama kisahani. |
| 10. | ERIC: | Ah! Hapo sasa. Njia tatu tafauti hebu eleza zaidi! |
| 11. | BELLA: | Hey, jamani mazungumzo yananoga tunakuwa kama tuko kwenye mahojiano ya redio! |
| 12. | DESIRÉE : | Hata mimi nafurahia sana. Najifunza pia! Endelea dada Bella. Hii Koili ya kwanza yaani IUD ina maana gani? |
| 13. | BELLA: | Kwa kimombo kirefu chake ni IntraUterine device – ndio maana kwa kifupi ikaitwa IUD, Koili hii ni ya shaba nayo huwa inatumbukizwa kwenye kizazi mahali ambapo hasa rutuba inapojengeka.Ni lazima daktari akuwekee Koili hiyo. Huwezi kufanya shughuli hiyo wewe mwenyewe. |
| 14. | DESIRÉE : | Na hiyo sijui Di.. Diaphramu? |

| | | |
|---|---|---|
| 15. | BELLA: | Ahaa..Hii pia ni koili lakini iko tafauti na IUD. Diaphragm inaumbo kama kisahani au kikofia cha plastik. Mama yake Eric alionyesha jinsi kujiweka mimi menyewe. Kisahani hiki unahitajika kukitumbukiza wewe mwenyewe kwa kutumia krimu spesheli. |
| 16. | ERIC: | Huwezi kukiacha kikofia hiki cha plastiki ndani. Lazima ukitoe halafu uweke tena krimu mpya kila wakati. Ni kama vile Kondomu – unatakikana kuitoa mara baada ya kuitumia. |
| 17. | BELLA: | Sawa sawa kabisa. Unajua sio rahisi kubadili krimu wakati wa hekaheka hizo na diaphramu inaongeza ghasia kwa sababu ya ile krimu. (laughing) nakwambia ilinitoka mkononi wakati mmoja! Kama samaki vile! Lakini wanawake wengine wanapendelea kuitumia. Wanasema eti huwezi kuhisi kama kuna kitu kigeni mwilini mwako. Pia haivurugi kabisa siku zako za mwezi yaani haibadilibadili siku zako unabaki vile vile kama kawaida. La muhimi ni kwamba unaitumia tu wakati unapo ihitaji kwa hivyo sio kitu kinachobaki mwilini mwako kabisa. Ni nafuu tena ni |

kinga ya muda mfupi sio kama sindano, au njia ya kupandikiza.

| | | |
|---|---|---|
| 18. | DESIRÉE : | Ok!  Je vipi kuhusu hizi njia zingine? |
| 19. | BELLA: | Habari ya kufurahisha ni kwamba wakati nilipokuwa nimesimama kwenye msitari kusubiri kuingia kwa daktari ili niwekewe Koili yaani- IUD- mwanamke mmoja aliyesimama karibu nami alianza kuzungumza. |

FLASHBACK  MUSIC

**Scene: In the clinic. Bella talks to a young woman in her early twenties.**

**SFX: FADE INTO CONVERSATION**

| | | |
|---|---|---|
| 20. | WOMAN : | Unajua gharama za njia tafauti za kuzuia ujauzito zinatafautiana sana. Unafahamu, utalipa kiasi gani? |
| 21. | BELLA: | Niliambiwa kuwa  gharama ya Koili kwanza ni kubwa.  Halafu unahitajika kurudi kliniki kuangaliwa katika kipindi cha mwaka mmoja kwa hivyo ukijumlisha gharama yote inakuwa chini ya dola  moja kwa mwaka, yaani ukiiangalia hesabu kwa kipindi cha miaka mitano.  Na yote hayo |

yameelezwa katika kijikaratasi cha maelezo.

| | | |
|---|---|---|
| 22. | WOMAN : | Oh! Natumai bei zinapungua kwa kuwa mahitaji yamekuwa makubwa sasa na pia kliniki nyingi kwa sasa zinatoa huduma za mpango wa uzazi. Mimi na mpenzi wangu tunatumia Kondomu, lakini sasa tumeamua tujaribu njia ya kupandikiza. |
| 23. | BELLA: | Oh! Sikuwa na habari kuwa njia hiyo inapatikana kwenye kliniki hii. |
| 24. | WOMAN : | Wanatoa huduma ya kupandikiza. Daktari atanipandikizia vijidude viwili kwenye ngozi chini ya mkono wangu yaani huku karibu na kwapani. Mimi ninaogopa kidogo lakini mpenzi wangu, Jordan, Yule pale ananipa moyo! |
| 25. | BELLA: | Ni vizuri. Je hukupendelea sindano? |
| 26. | WOMAN : | La sikupendelea. Lakini baadhi ya marafiki zangu huwa wanakuja kudungwa sindano kila baada ya miezi mitatu. Madaktari wanashauri matumizi ya Kondom iwapo mtu ana mpenzi zaidi ya mmoja. Jordan na mimi tunaamini mtu kuwa na mpenzi mmoja tu. |

| | | |
|---|---|---|
| 27. | BELLA: | Pia mimi na Robert tuna amini hivyo. Hata hivyo tunapima HIV kila mwaka. Ukweli ni kwamba yoyote kati ya wapenzi anaweza kuteleza hasa katika makamo yetu haya. Ndoa sio kithibitisho. Mtu anaweza kulewa kupita kiasi mara moja tu katika Party halafu.....mimi nadhani lazima tuwe waangalifu sana siku hizi au wewe unaonaje? |
| 28. | WOMAN: | Usemayo ni kweli kabisa. Na unaposema kuhusu gharama, uzazi na kuwa na watoto pia gharama kubwa! Sisi tumeamua kupata watoto wakati ambapo tutakuwa tuna akiba ya kutosha. |

END OF FLASHBACK MUSIC UP AND OUT
INSERT NEW SECTION

**NARRATOR:** Bella na mdogo wake, Desirée, waliendelea kuzungumza huku Eric akiandika maelezo yale kwa ajili ya utafiti wake. Alikuwa amejifunza mengi mpaka sasa kuhusu kwa nini wanawake walipendelea njia Fulani za kupanga uzazi kuliko zingine. Pia alifahamu kwa nini Bella alichagua Koili. Alifahamu pia umuhimu wa Mume au mwenza katika kufanya maamuzi. Wakati huo huo nyumbani kwao mjini Kentown, dada yake, Lorraine alikuwa na matatizo tafauti katika mawazo yake. Alikuwa anayajadili matatizo hayo na mpenzi wake Sazi.

29. SAZI: (Irritated) Nilijua kuna jambo! Ni siku ngapi sasa umekuwa unajisikia namna hii?

30. LORRAINE: (Upset)Siku nane – au tisa , oh hata sijui vizuri. Nilikuwa mgonjwa kweli wakati nilipokuwa kwenye majaribio kwa Bongo. Hata sijui alinifikiriaje! Nilipokuwa narudi nyumbani nilipitia kwenye duka la dawa na nikanunua kipima mimba. Jana usiku sikuonyesha dalili zozote za kuwa nina mimba.

31. SAZI: Kwa hivyo? Ni kitu gani kinachokutia wasiwasi?

32. LORRAINE: Kwa sababu ninajisikia tafauti. Na pia nimesoma kuwa mwanamke anaweza kupata matokeo kuwa hana mimba kwa sababu homoni huwa bado ziko katika hali ya mabadiliko. Sasa leo asubuhi nilipima tena kabla sijanywa kitu chochote.

33. SAZI: Halafu?

34. LORRAINE: Imeonyesha kuwa nina mimba!

35. SAZI: Lakini jana mchana ulikuwa huna kitu ila leo asubuhi imeonyesha una mimba?

Pengine ukipima tena itaonyesha huna mimba!

36. LORRAINE: Hebu – soma maelezo haya wewe mwenyewe!

37. (SFX Paper)

38. SAZI: (Reading) "Ni vizuri kukusanya mkojo ulio na homoni nyingi zinazoweza kuonyesha chembechembe za dalili za mimba". (Changing voice/softer) , blah blah..oh hapa- (Reading again) " Matokeo ya Mkojo wa kwanza asubuhi yanaweza kuaminika kwa sababu homoni nyingi ambazo hazijachanganyika hupatika katika mkojo huo." (Normal voice) Ok. Kwa hiyo sasa ni hakika kuwa una mimba, kutokana na matokeo ya asubuhi ya leo?

39. LORRAINE: Jana sikuwa na uhakika, lakini leo asubuhi kila kitu kilijionyesha wazi . (sobbing) Nina mimba Sazi!

40. SAZI: Oh! Vipi itokee hivi? Labda ulikosa kumeza tembe zako mara nyingi tu. Kwa nini sikutumia Kondom jamani. Kwanini!

41. MUSIC UP

42. NARRATOR: Desirée, dada yake, Bella na Eric walikuwa wanafikia mwisho wa

| | | |
|---|---|---|
| | | mazungumzo yao. Eric alidhani kuwa angeweza pia kumuhoji nyanya kuhusu njia za kienyeji za mpango wa uzazi. Lakini alipoingia ndani Eric aligundua mara moja kuwa haingewezekana.. |
| 43. | GRANMA: (strict) | Wanangu mnazungumzia nini lakini, uh? Eric, umekuwa hapa kwa muda mrefu. Kitu gani kinachoendelea hapa? |
| 44. | ERIC: | Nyanya Linda. Tunazungumzia juu ya mradi wa utafiti. |
| 45. | GRANMA: | Unafanya utafiti gani na wasichana wangu? Hey? |
| 46. | ERIC: (unsure ) | Um..wajua..mimi ninakuja hivi karibuni kuishi hapaI Mtelera nitakuwa nafanya kazi katika kliniki mpya ya hapa. Mama yangu ndiye atakuwa msimamizi wa kliniki hiyo.. um.. |
| 47. | GRANMA: | Na yeye anaamini mpango wa uzazi. Lakini sisi hatuamini. Sisi wanakijiji wa Mtelera tunataka kliniki kwa ajili ya matibabu ya kawaida tu. |
| 48. | 6. ERIC: | Bila shaka yatakuwepo.  Lakini wanawake wanataka kujua… |

49. GRANMA (Interrupts) Wanawake wanataka kujua nini? Kujifanya kama wanawake wa kizungu? Namna ya kudhibiti idadi ya waafrika? Huu Mpango wa Uzazi. Bah! Unabadili kabisa maisha yetu.

50. BELLA: MAISHA yetu, nyanya Linda. Ndio kweli, Siyo yako. Sisi tunataka mabadiliko na tunataka kuwa miongoni mwa mabadiliko hayo. Ai! masikini Mama (sobbing), ;laiti angekuwa na nafasi ya kuchagua ni wakati gani wa kupata mtoto, angekuwa hai bado. (wailing) Oh Mama! Mimi sitaki kupata yaliyokufika wewe!

51. Sobbing intermittently FADE UNDER

**NARRATOR:** Huku ameshikilia dada yake, Desirée alimbembeleza kwa kumpapasa nywele zake. Hii ilikuwa ni mara yao ya kwanza kumlilia mama yao pamoja tangu alipofariki. Eric na Nyanya walikaa kimya huku wakiwaagnalia. Desirée alimwibia dada yake wimbo alioupenda sana mama yao mpaka alipopata usingizi.

**OUTRO.**

Ni hayo tu kwa leo kutoka kwenye Noa Bongo Jenga Maisha Yako. Ulikuwa ukiusikiliza mchezo kwa jina Chini Ya Miembe. Mchezo ulioandikwa na Romie Singh.

Jiunge nasi katika sehemu ya tisa ambapo kile alichokuwa akikiogopa Lorraine kinajitokeza wazi, Desirée anazidisha juhudi za kuwatafura baba yake na mjomba wake.
Kumbuka iwapo unataka kuusikiliza tena mchezo huu au kumwambia rafiki yako juu ya mchezo huu wa kusisimua, tafadhali usikilize kupitia kwenye mtandao wetu. Na anuani yenyewe ni: d w world dot de mkwaju l b e
Hadi wakati mwingine, Kwaheri.

**END OF EPISODE EIGHT**